

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA NANE

10 FEBRUARI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA NANE – TAREHE 10 FEBRUARI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:


IV. MASWALI YA KAWAIDA:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

81. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatumiaje Chuo cha Bahari cha (DMI) kuendeleza Vijana wa Kitanzania ili kukabiliana na changamoto za ajira.



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

82. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini kinakwamisha ujenzi wa stendi mpya ya Geita Mjini na lini sasa ujenzi huo utanza.

**83. MHESHIMIWA ISSA ALLY MCHUNGAHELA
(LULINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Vituo vya Afya vya Nagaga na Mnavira vitakamilika.

WIZARA YA MAJI:

**84. MHESHIMIWA EDWARD KISAU
OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:

Je, ni lini ahadi iliyotolewa wakati wa Kampeni za Urais ya ujenzi wa Mabwawa mawili ya Maji katika Wilaya ya Kiteto itatekelezwa.

WIZARA YA NISHATI:

**85. MHESHIMIWA MASACHE NJELU KASAKA
(LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-


Je, ni lini Serikali itafikisha umeme kwenye Vijiji ambavyo bado havijafikiwa Wilayani Chunya pamoja na Makao Makuu ya Kata za Nkung'ungu, Lualaje, Mafyeko na Kambikatoto.

WIZARA YA AFYA:

86. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje katika kupunguza ama kumaliza kabisa changamoto ya ukosefu wa Dawa katika Vituo vya kutolea huduma za Afya nchini.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

87. MHESHIMIWA JOHN MARKO SALLU (HANDENI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Kwamsisi mpaka Mkata kwa kiwango cha lami.

**88. MHESHIMIWA DAIMU IDD MPAKATE
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mtwarapachani, Lusewa, Nalasi hadi Tunduru yenye urefu wa Km 320 kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**89. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA
(CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itafanya ziara kwenye Vituo vya Polisi vya zamani na nyumba za kuishi Askari Unguja na Pemba ili kushuhudia uchakavu uliopo na ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya Vituo vya Polisi nchini kwa Mwaka 2021/2022.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

90. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka dirisha maalum la Vijana kwenye kila Benki za Serikali nchini ili kuwawezesha Vijana kupata mitaji na mikopo yenye riba nafuu.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

91. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha masomo ya ziada ya kazi za mikono kama vile, useremala, mapishi, kushona, kilimo, ujenzi katika Shule za Msingi na Sekondari ili kupunguza changamoto ya ajira.

V. HOJA ZA KAMATI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

MWENYEKITI WA KAMATI KUDUMU YA BUNGE YA MASUALA YA UKIMWI:

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2021.

DODOMA
10 FEBRUARI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE